**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Sudan**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير

HIZB UT TAHRIR

**Jumatatu, 27 Shawwal 1445 H** **06/05/2024 M** **Na: HTS 1445 / 35**


# Taarifa kwa Vyombo vya Habari

## Hizb ut Tahrir / Wilayah Sudan Yakutana na Viongozi wa Harakati ya Islamic Action (Imetafsiriwa)

Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir/Wilayah ya Sudan, ukiongozwa na Ustadh Nasser Ridha, Mkuu wa Kamati Kuu ya Mawasiliano ya Hizb ut Tahrir katika Wilaya ya Sudan, na wanachama Ustadh Abdullah Hussein, Mratibu wa Kamati Kuu ya Mawasiliano, na Ustadh Muhammad Mukhtar, Mwanachama wa Hizb ut Tahrir, alikutana na idadi ya viongozi wa Harakati ya Islamic Action katika afisi ya Hizb mjini Port Sudan, Jumapili, 26 Shawwal 1445 H sawia na 05/05/2024. Mkutano huo ulihudhuriwa na viongozi wa harakati hiyo ya Kiislamu:

1- Dkt. Abdullah Al-Ardab

2- Sheikh Yasser Bashir

3- Sheikh Al-Khair Al-Obaid

4- Dkt. Zuhair Abdel Rahman

5- Dkt. Zuhair Salah El-Din.

Mkutano huo ulijadili wasiwasi jumla nchini humu, mzozo wa kijeshi unaoendelea nchini Sudan, na uingiliaji kati wa dola za nje na usimamizi wao wa vita hivi, ili kuwezesha mradi wa makafiri wa Magharibi wa kuifanya nchi hii kuwa ya kisekula, kuigawanya na kuivunja vunja. katika vidola dhaifu. Pande hizo mbili ziliafikiana jinsi ya kukabiliana na njama hizi kupitia juhudi za pamoja za wabebaji da'wah, kupitia kueneza ufahamu miongoni mwa umati wa uhalisia wa mpango wa nchi za kikoloni, na ufahamu wa mradi wa kuunganisha Umma unaowakilishwa na kusimamisha chombo kinachounganisha Ummah chini ya Dola ya Khilafah, na kwamba Hizb ut Tahrir/Wilayah Sudan iko katika mchakato wa kufanya kongamano la kujadili masuala ya nchi, na kwamba suluhisho linatoka ndani ya Aqidah (itikadi) ya Kiislamu na sio kwa kuomba masuluhisho ya nje kutoka kwa nchi za kikoloni zenye ulafi katika nchi yetu.

Kwa upande wao viongozi wa Islamic Action wamesisitiza kuwa, suluhisho linapaswa kuegemezwa kwenye Aqida tukufu ya Uislamu, na kufanya kazi ya kuwa kitu kimoja kukabiliana na mipango muovu wa kikoloni, na kwamba wako tayari kufanya kazi katika mwelekeo huu.


**Ibrahim Othman (Abu Khalil)**
**Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir**
**katika Wilayah Sudan**



**Simu:** 0912240143- 0912377707

**Pepe:** Spokman_sd@dbzmail.com

**Tovuti:** www.hizb-sudan.org

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.org

**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.info